# SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
# WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO

## HOTUBA YA BAJETI YA WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO

## MHESHIMIWA TABIA MAULID MWITA (MBM)
## KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2025/2026

**MEI, 2025**

**YALIYOMO**

A. UTANGULIZI ........................................................ i

B. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 ........................................ 1

C. UPATIKANAJI WA FEDHA 2024/2025 ........................... 3

D. MAFANIKIO YA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 ........................................................ 3

E. MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 ........................................................ 22

F. MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 ... 28

G. MWISHO ........................................................ 29

VIAMBATANISHO. ................................................ 30

**HOTUBA YA BAJETI YA WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO, MHESHIMIWA TABIA MAULID MWITA (MBM) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA 2025/2026**

## A. UTANGULIZI

**1.Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako likae kwa madhumuni ya kupokea, kujadili na kupitisha utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na kuidhinisha Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kwa Wizara ya Habari,Vijana,Utamaduni na Michezo.

**2.Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia kuwepo hapa tukiwa katika afya njema na furaha. Namuomba Allah (S.W) aendelee kutudumisha katika amani na utulivu nchini kwetu. Atuzidishie imani thabiti ya kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025 katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar ilikufikia maendeleo yaliyokusudiwa.

**3.Mheshimiwa Spika,** napenda kumpongeza kwa dhati **Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar** na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake makini na mahiri anaouonesha katika kuiongoza Zanzibar na kuiwezesha kupata mafanikio makubwa katika sekta zote za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Vile vile, pongezi niendelee kwake kwa kuitekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025 kwa asilimia kubwa pamoja na kuiendeleza Zanzibar kuwa kitovu cha amani na utulivu. Nimuahidi kuwa nitaendelea kumpatia mashirikiano ya dhati kabisa katika kutekeleza majukumu yake ya kuiendele za Zanzibar.

**4.Mheshimiwa Spika,** nampongeza **Mheshimiwa Othman Masoud Othman,** Makamo wa kwanza wa Rais wa Zanzibar kwa ushirikiano anaoendelea kuutoa kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar. Vile vile, nampongeza **Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla,** Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar, kwa kuendelea kuratibu na kusimamia shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya

Zanzibar katika Baraza lako Tukufu na kumsaidia Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika Utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025.

**5.Mheshimiwa Spika,** naomba nikupongeze wewe binafsi na Naibu Spika pamoja na wenyeviti wa Baraza kwa kuliongoza Baraza hili tukufu kwa umakini na umahiri wa hali ya juu katika kufikia maamuzi mbalimbali yenye manufaa kwa ustawi wa Wazanzibari. Tunawaambia kuwa juhudi zenu tunaziona na kuzithamini.

**6.Mheshimiwa Spika,** shukrani zangu za dhati kabisa ziende kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kwa maoni, ushauri na mapendekezo mazuri wanayotupatia kila tunapokutana kujadili utekelezaji wa majukumu ya Wizara yetu. Aidha, nawashukuru wajumbe wa kamati za Baraza kwa mashirikiano mbalimbali wanayotupatia wakati wa kuandaa bajeti yangu ya mwaka 2025/2026. Napenda kuwahakikishia Kamati na Baraza lako tukufu kuwa maoni na mapendekezo yaliyotolewa yamezingatiwa na kufanyiwa kazi katika bajeti hii.

**7.Mheshimiwa Spika,** naomba nichukue fursa hii kuwashukuru Mawaziri wenzangu na wajumbe wote wa Baraza hili tukufu kwa ushirikiano mnaonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu. Nidhahiri kwamba mashirikiano baina yetu ni nguzo muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa CCM, mipango na mikakati ya kitaifa katika kuleta maendeleo na kukuza uchumi na hali za maisha ya wananchi wa Zanzibar,

**8.Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo sasa naomba kuwasilisha Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na mwelekeo wa Bajeti ya mwaka 2025/2026 kama ifuatavyo:

## B. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**9.Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2024/2025, imetekeleza Programu kuu nne na programu ndogo nane chini ya Fungu J03 na Fungu J05. Programu Kuu hizo ni kama zifuatazo:

**Programu ya Maendeleo ya Habari, Utangazaji na Uchapaji;**
**Programu ya Maendeleo ya Vijana;**
**Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo; na**
**Programu ya Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.**

## C. UPATIKANAJI WA FEDHA ZA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU NA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**Fungu [illegible]:Wizara ya Habari,Vijana ,Utamaduni na Michezo**

**10.Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo iliidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 89,291,932,000/-** kwa ajili ya utekelezaji wa programu. Kati ya hizo **shilingi bilioni 19,067,950,000/-** na **shilingi bilioni 70,223,982,000/-** kwa miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2025 Wizara ilifanikiwa kupata **shilingi bilioni 85,249,095,540/-** sawa na asilimia **95** ikiwa **shilingi bilioni 12,309,547,865/-** kwa matumizi ya kazi za kawaida sawa na asilimia **65** na **shilingi bilioni 72,939,547,675/-** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na asilimia **104. Kiambatanisho nambari 1A kinahusika.**

**11.Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa ukusanyaji wa mapato, Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya **shilingi milioni 575,000,000/-** na hadi kufikia Machi, 2025 Wizara imefanikiwa kukusanya **shilingi milioni 283,991,550** sawa na asilimia 49 ikiwa ni mapato ambayo yanaingia Mfuko Mkuu wa Serikali. **Kiambatanisho 1B kinahusika.**

## D. MAFANIKIO YA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**Programu Kuu Maendeleo ya Habari, Utangazaji na Uchapaji**

**12.Mheshimiwa Spika,** Programu hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 10,394,556,000/-** kwa matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Machi,2025 Programu hii iliingiziwa **shilingi 6,166,380,338** sawa na asilimia **59 Kiambatanisho nambari 1A kinahusika.**

**13.Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Idara ya Habari Maelezo imefanikiwa kuandaa na kusambaza taarifa **1,146** za matukio mbalimbali kwa wananchi kupitia vituo vya habari vya umma na binafsi. Pia, taarifa hizo zilitumwa kwenye mitandao ya kijamii ya Idara ya Habari Maelezo ili wananchi waweze kupata taarifa za matukio yanayojiri kwa urahisi. Vile vile, Wizara imefanikiwa kuuza picha rasmi za Viongozi Wakuu wa nchi **349** zikiwemo picha **137** za Rais wa Zanzibar, picha **182** za Rais wa Jamuhuri ya Muungano ya Tanzania na picha **30** za Rais Wastaafu.

**14.Mheshimiwa Spika,** Katika hatua ya kusimamia na kuwawezesha wanahabari kufanya kazi zao bila ya vikwazo, Wizara imetoa vitambulisho 184 vya waandishi wa habari sambamba na vibali **11** vya uchukuaji wa picha za kutengenezea makala na filamu. Jumla ya wanahabari 128 kutoka SMZ na SMT walishiriki mafunzo maalum ya siku 3 yaliyofanyika katika Ukumbi wa New Amaan Comlex. Kupitia mafunzo hayo yaliyoratibiwa na Serikali (SMZ), TAMWA na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, waandishi na Maafisa Habari wamejengewa uwezo wa kutoa taarifa zenye viwango, sahihi na kwa wakati zinazohusiana na Maendeleo ya nchi sambamba na utekelezaji wa Sera na Mipango ya Serikali.

**15.Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa programu hii umeiwezesha ZBC kuandaa vipindi **4,370** kupitia TV, vipindi **8,250** kupitia Redio na vipindi **2,346** kupitia Spice FM. Sambamba na utayarishaji na urushaji wa matangazo mbali mbali **30,375** na matangazo ya moja kwa moja **318.** Vile vile, Shirika la Utangazaji Zanzibar limefanikiwa kuanzisha vipindi vipya vya TV vikiwemo Ijue Mahakama; Kamisheni ya Ardhi na Mwangaza.

**16.Mheshimiwa Spika,** kwa kushirikiana na wadau na Taasisi nyengine za Serikali, ZBC imefanikiwa kuratibu matukio matano (5) ambayo ni Mashindano ya kombe la Yamle Yamle, kampeni ya Mkono kwa Mkono, Minne kama 400, Vumba Festival na Mashindano ya kuhifadhi Qur-an Tukufu ya Afrika. Kupitia matukio hayo ZBC imepata fursa ya kujitangaza ndani na nje ya nchi.

**17.Mheshimwa Spika,** mafanikio mengine yaliyopatikana katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara kupitia Kampuni ya

Uunganishaji na Usambazaji wa Maudhui (ZMUX) imefanikiwa kununua **Back Up** mbili zenye thamani ya **Shilingi milioni 111,100,000/-** kwa ajili ya vituo vya Masingini Unguja na Chakechake kwa Pemba. Zenye lengo la kuondosha tatizo kukatika maudhui (signal) wakati wa kukatika kwa umeme. Sambamba na hilo ZMUX katika kuhakikisha huduma na bidhaa zinawafikia wananchi wa Unguja na Pemba, Kampuni imefanikiwa kufanya kampeni maalum iliyoitwa **"Funga Mwaka na ZMUX"** ambapo ving'amuzi 460 (331 Unguja na 129 Pemba) ikiwa lengo lake lilikuwa ni kuwashajihisha, kuwaelimisha na kuwapatia ving'amuzi vipya wananchi pamoja na kuwatatulia changamoto zao zinazowakabili katika vingamuzi vyao. Jumla ya wananchi 1437 wamefikiwa na kampeni hiyo (814 Unguja na 623 Pemba).

**18.Mheshimwa Spika,**Katika kuboresha vipindi vinavyorushwa ZMUX kupitia chanali zake za ZMUX Swahili na ZMUX Taqwa. Kampuni imefanikiwa kutayarisha na kurusha hewani Tamthilia mpya ya **"MAISHA"** Pamoja na kuongeza vipindi kama vile Tambo za Mwambao, Safari ya Maendeleo, Haiba ya Ramadhani, Madrasa zetu Pamoja na ***Live Request.*** Vipindi hivi vitasaidia kuelimisha na kuwaburudisha wananchi.

**19.Mheshimwa Spika,** katika kuwaendeleza wafanyakazi kuendana na sayansi na teknolojia ZMUX imefanikiwa kuwasomesha wafanyakazi wawili mafunzo ya muda mrefu katika fani za *Master of Science in Information Technology* katika chuo cha SUZA na *Diploma in Secretarial Information and Office Management* katika chuo cha **KIU** Uganda. Aidha wafanyakazi wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani (short courses) za: *Accrual Basis, IPSAS's, Store Management Records, Kuhusu Kustaafu, NMX Server Configurations, Monitoring and Operations, TSE Configurations' and Set UP Exciters Operation Configurations and Management, Automation of Back UP and its Operation, Customer Care na Power Inverter, Back Up and Ups Design, Installation and Maintenances*

**20.Mheshimiwa Spika,** Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar (SMS) linaendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kuchapisha magazeti na kuyasambaza Zanzibar na Tanzania Bara kwa lengo la kutoa habari zenye kuelimisha na kuburudisha. Jumla ya nakala **942,000** za Magazeti zimechapishwa na kusambazwa yakiwemo matangazo **3,082** Habari na Makala **13,734.** Aidha, Shirika limefanikiwa kuchapisha nakala **2,000** za Jarida la **Neema Zetu** lenye lengo la kuwahabarisha wananchi juu ya Neema za Serikali ya Awamu ya Nane.

**21.Mheshimiwa Spika,** Shirika la Magazeti limefanikiwa kwenda kidigital kulingana na mabadiliko ya teknolojia ya habari ambapo kwa sasa magazeti ya Shirika yanapatikana kwa njia ya mitandao ya kijamii na website ya Shirika, www.smsz.co.tz, ambapo hupelekea kazi za Shirika kujulikana zaidi na wananchi kupata habari muhimu zinazohusu maendeleo ya nchi.

**22.Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar umepokea kazi za uchapaji **948** zenye thamani ya **shilingi bilioni 1.85** kutoka taasisi za Serikali na binafsi ambapo kazi zote hizo zimekamilika kwa asilimia **100.** Aidha, wakala umechapisha magazeti rasmi ya Serikali **252**, mitihani ya kidato cha pili, Darasa la saba na Darasa la nne ya Baraza la Mitihani Zanzibar kwa ufanisi, usiri na kuiwasilisha kazi hiyo kwa wakati. Vile vile, Wakala wa uchapaji unaendelea kutoa huduma za bohari kuu ya vifaa vya ofisi na kuandikia kwa taasisi za Serikali na binafsi, jumla ya maombi **63** yenye thamani ya **shilingi milioni 188.58** yalipokelewa nakupatiwa huduma.

**23.Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha utendaji wa kazi, Wakala wa Uchapaji umenunua mitambo mipya **2** na kuifanyia matengenezo mitambo **39** kwa kutumia mafundi wake wa ndani. Aidha, katika kuimarisha mazingira bora ya kazi wakala umeendelea na ujenzi wa ofisi kwa awamu ya pili ambapo jengo hilo kwa sasa limefikia asilimia 85.

**Programu ya Maendeleo ya Vijana.**

**24.Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2024/2025,** Programu hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 5,662,714,000/-** kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 1,162,714,000/-** ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na **shilingi 4,590,000,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2025 programu hii, imeingiziwa jumla ya **shilingi milioni 681,317,417/-** sawa na asilimia 12 kati ya hizo shilingi milioni 561,787,417/- sawa na asilimia 48 ni matumizi ya kazi za kawaida na **shilingi milioni 119,530,000/-** sawa na asilimia **3** ya miradi ya maendeleo. **Kiambatisho namba 1A kinahusika.**

**25.Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana kupitia programu hii ni kusimamia na kuratibu utekelezaji wa sera, mipango na programu za kitaifa za Maendeleo ya vijana nchini. Wizara kwa kushirikiana na wadau wa Maendeleo ya Vijana imefanikiwa kuchapisha nakala **3,600** za Sera ya Maendeleo ya Vijana Zanzibar. Kati ya nakala hizo, jumla ya nakala **2,944** zimesambazwa kwa makundi mbali mbali ya Viongozi, Watendaji wa Serikali, Asasi zisizo za Kiserikali na Vijana.

**26.Mheshimiwa Spika,** Jumla ya vijana 325,435 (Unguja 212,018 na Pemba 113,417) wakiwemo wanawake 186,412 na wanaume 139,023 wamefaidika kupatiwa mafunzo mbali mbali yakiwemo; Stadi za Maisha, Ujasiriamali, Stadi za Kazi, Afya ya Uzazi, Uongozi na Uzalendo, Ushiriki na Ushirikishwaji, Mabadiliko ya Tabia ya nchi, Amani na usalama na mafunzo ya TEHAMA. Mafunzo hayo yalitolewa kwa ushirikiano mkubwa na wadau wa Maendeleo ya Vijana wakiwemo Shirika la UNFPA, YCI na T-MARC kupitia mradi wa Kijana Nahodha, Zanchange Makers, Wizara ya Afya, Tume ya Mipango na Wizara ya Kilimo.

**27.Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Vituo vya Mafunzo ya Vijana hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya vijana 1,866 (Mwanamke 1,053 na Mwanamme 813) wamefikiwa Unguja na Pemba. Kwa upande wa kituo cha Bweleo Unguja jumla ni vijana 1,294 (Mwanamke 711 na Mwanamme 583) na kituo cha Weni Pemba jumla ni vijana 572 (Mwanamke 342 na Mwanamme 230). Mafunzo hayo yalihusisha mada za Uongozi, Stadi za Ajira, Afya ya Uzazi, Udhalilishaji wa Kijinsia, Ufugaji, Ushoni, Ufundi

wa Aluminium, Upambaji, TEHAMA na Mchezo wa Karate, Na yalitolewa kwa Mashirikiano na wadau wa Maendeleo ya Vijana wakiwemo Shirika la UNFPA, YCI, T-MARC kupitia mradi wa Kijana Nahodha, Zanchange Makers, Wizara ya Afya, Tume ya Mipango na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Mali ya Asili na Mifugo Zanzibar.

**28.Mheshimiwa Spika,** sambamba na hayo, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa Maendeleo ya Vijana Zanzibar imefanikiwa kutembelea jumla ya vikundi 297 vya kiuchumi (Unguja 147 na Pemba 150) ikiwa ni pamoja na kuvipatia ushauri wa kitaalamu, mafunzo na kuwaunganisha na fursa mbali mbali za uwezeshaji. Wizara inaendelea kufanya uhamasishaji kwa Vijana kujiunga na Vikundi vya kiuchumi ambapo jumla ya vikundi 228 vipya vya kiuchumi (Unguja 82 na Pemba 146) vilianzishwa, kusajiliwa na kuunganishwa na fursa za Mikopo. **Kiambatanisho 2 kinahusika**

**29.Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mikopo ya uwezeshaji, jumla ya vikundi 119 vya Vijana (Unguja 57 na Pemba 62) vimewasilisha maombi yao ya mikopo kwa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (ZEEA) yenye thamani ya **shilingi TZS bilioni 2.09** ambapo kati ya hivyo vikundi 24 vimeshapatiwa mikopo yenye thamani ya **shilingi milioni 294** na vikundi 95 vipo katika mchakato wa kukamilisha taratibu za maombi. Aidha Taasisi ya Aslan Development Foundation imeweza kuwapatia mikopo vikundi vitatu vya Vijana yenye thamani ya **shilingi milioni 9.0.**

**30.Mheshimiwa Spika,** Jumla ya fedha taslimu **shilingi milioni 50.3** na vifaa vya uzalishaji vyenye thamani ya **shilingi milioni 189.93** vimetolewa kwa vikundi 32 na vijana mmoja mmoja 169 Unguja na Pemba. Vifaa na fedha hizo zimetolewa na wadau wa maendeleo ya Vijana wakiwemo USAID, Feed the Future, Uchumi wa Buluu, SOS, PIRO, Viongozi wa majimbo pamoja na Idara ya Maendeleo ya Vijana yenyewe**. Kiambatanisho namba 3A kinahusika**

**31.Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo ya Vijana Nchini imeadhimisha Siku ya Vijana Kimataifa tarehe 12 Agost, 2024. Maadhimisho hayo yalifanyika kitaifa katika Ukumbi wa Goden Tulip Uwanja wa Ndege Zanzibar

na kushirikisha Viongozi, Wadau na Vijana kutoka taasisi mbali mbali za Maendeleo ya Vijana Nchini. Mgeni rasmi katika maadhimisho hayo alikuwa ni Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Ujumbe wa Mwaka 2024 ulikuwa **"Kijana! Songa Kidijitali kwa Maendeleo Endelevu".** Aidha, maadhimisho hayo yaliambatana na shughuli mbalimbali zikiwemo; Usambazaji wa Sera na utoaji wa elimu juu ya Sera mpya ya Maendeleo ya Vijana Zanzibar ya mwaka 2023, makongamano yaliyojadili fursa za Uwezeshaji na ushiriki wa Vijana, usafi wa Mazingira na usiku maalum wa Vijana ulioshirikisha sanaa na burudani mbali mbali za Vijana Zanzibar. Jumla ya Vijana 3,364 walishiriki Maadhimisho hayo. **Kiambatanisho namba 3B kinahusika**

**32.Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na UNICEF kupitia programu ya U-report ilifanya ziara katika maeneo mbali mbali ya kushajihisha vijana wa vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu kujiunga na jukwaa la mtandaoni (U-report). Lengo la programu hiyo ni kuimarisha ushiriki na ushirikishwaji wa Vijana katika mambo yanayowahusu kupitia Majukwaa ya mtandaoni. Hadi kufikia Machi, 2025 zaidi ya vijana 25,000 Unguja na Pemba wameshajiunga na programu hiyo.

**33.Mheshimiwa Spika,** Katika kuhamasisha umoja, amani, upendo na maendeleo nchini, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu Tanzania imeendelea kuratibu na kusimamia Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa kwa kufanikisha Kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru, Kumbukumbu ya Baba wa Taifa, Mw. Julius K. Nyerere, na Wiki ya Vijana Kitaifa kwa Mwaka 2024 kilichofanyika Mkoani Mwanza. Jumla ya Miradi 78 ya Maendeleo katika Sekta ya Afya, Elimu, Maji, Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi, Maendeleo ya Vijana, Barabara na Uhifadhi wa Mazingira yenye thamani ya **shilingi bilioni 417.9** ilitembelewa, kukaguliwa, kuwekewa Mawe ya Msingi na Kuzinduliwa kwa upande wa Zanzibar. Aidha Wizara iliratibu maandalizi ya Wiki ya Vijana Kitaifa iliyofanyika Mkoani Mwanza kuanzia tarehe 8 Oktoba - 14 Oktoba 2024 ambapo jumla ya Vijana 20 (wanawake 11 na 9 Wanaume) walishiriki katika maonesho ya kazi za Vijana na makongamano yaliyojadili fursa za uwezeshaji, Sera ya Maendeleo ya Vijana na Ushiriki na

Ushirikishwaji wa Vijana.
Pia Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu imefanikiwa kuratibu shughuli ya Uzinduzi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa kwa Mwaka 2025 uliofanyika tarehe 02/04/2025 Mkoani Pwani ambapo Mgeni Rasmi wa uzinduzi huo alikuwa Dkt. Philip Isidor Mpango Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ujumbe wa mwaka huu ni ***'' Jitokeze Kushiriki Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 kwa Amani na Utulivu''. Kiambatanisho 3C kinahusika***

**34.Mheshimiwa Spika,** Baraza la Vijana Zanzibar limeendelea kuhamasisha Vijana kujiunga na Baraza la Vijana kupitia vyombo vya habari na ziara za kiutendaji. Jumla ya Vijana **1,083** wameshajihishwa, kati ya hao Vijana **295** wamejiunga na Baraza la Vijana. Aidha, Baraza limefanikiwa kufanya kikao kazi cha watendaji wakuu katika ngazi za Wilaya Unguja na Pemba. Kikao hicho kilijadili changamoto mbali mbali na namna ya kuzitatua sambamba na kuzindua kampeni ya ***'Imarisha Mabaraza ya Vijana Zanzibar'.***

**35.Mheshimiwa Spika,** Baraza la Vijana Zanzibar limefanikiwa kuwajengea uelewa Vijana **1,396** juu ya kuwa wazalendo na kuipenda nchi yao kwa kushiriki katika matukio mbali mbali ya kitaifa. Aidha, Baraza limeweza kushiriki katika shughuli mbali mbali za kitaifa ikiwemo maadhimisho ya siku ya Vijana kimataifa, Maonyesho ya siku ya wakulima duniani, sherehe za miaka 61 ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar, kushiriki Tamasha la Vitabu Zanzibar, kushiriki katika uzinduzi wa Mradi wa Vijana Plus uliofanyika Dar es Salam na kushiri katika Mkutano wa United Nations population Fund nchini Angola.

**36.Mheshimiwa Spika,** Baraza la Vijana Zanzibar kwa kushirikiana na taasisi ya SOS imefanikiwa kuanzisha programu ya **MOBILE YOUTH SPACE (MYS)** kupitia Wilaya zote za Unguja na Pemba. Lengo la programu hiyo ni kuwawezesha vijana kushiriki na kushirikishwa katika mambo mbali mbali na kuweza kusikika sauti zao kwa uharaka. Kadhalika, Baraza limefanikiwa kufanya uzinduzi wa Kampeni ya **'AMANI NI TUNU, VIJANA TUIENZI'.** Lengo la kampeni hiyo ni kudumisha amani katika uchaguzi Mkuu

wa mwaka 2025 na baada ya uchaguzi. Pia, Baraza limeanzisha programu ya Future Hub yenye lengo la kuimarisha ushiriki wa Vijana wa Zanzibar katika nganzi ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

***Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.***

**37.MheshimiwaSpika,**kwamwakawafedha2024/2025,Programu hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 69,216,860,000/- kati ya hizo **shilingi bilioni 3,582,878,000/-** kwa matumizi ya kazi za kawaida na **shilingi bilioni 65,633,982,000/-** kwa miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2025 Wizara imeingiziwa jumla ya **shilingi bilioni 2,547,015,317/-** sawa na asilimia 71 kwa matumizi ya kawaida na **shilingi bilioni 71,531,944,479/-** sawa na asilimia 109 kwa miradi ya Maendeleo. **Kiambatisho nambari 1A na 1D kinahusika**

**38.Mheshmiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kufanya Tamasha la **29** la Utamaduni wa Mzanzibari kwa lengo la kurithisha mila, silka, desturi na Tamaduni za Mzanzibari. Shughuli mbali mbali zenye mnasaba na tamasha hilo zilifanyika zikiwemo maonyesho ya bidhaa za kitamaduni na madawa ya asili, sanaa za ngoma za asili na paredi ya wasanii na wajasiriamali iliyosheheni vionjo vya kitamaduni. Vile vile, Serikali iliruhusu kufanyika kwa matamasha ya kijamii yakiwemo Tamasha la Mwaka Kogwa, ZIFF na Tamasha la Sauti za Busara kwa lengo kuhamasisha jamii kuendeleza, kulinda na kurithisha mila, silka, maadili na Utamaduni wa Mzanzibari. Pia, Wizara imesaidia vikundi **78** vya kitamaduni na wasanii **28** kushiriki katika matamasha mbali mbali ndani na nje ya nchi.

**39.Mheshmiwa Spika,** Serikali inaendelea kuchukuwa juhudi kubwa za kuielimisha jamii juu ya umuhimu wa kuendeleza sanaa na utamaduni wa Kizanzibari. Sambamba na hilo, Serikali inatoa wito kwa viongozi wa dini, walimu, wazazi na walezi kila mmoja kwa nafasi yake kushiriki kikamilifu katika kuwaelimisha watoto na vijana juu ya umuhimu wa kufuata maadili mema na kujiepusha na vitendo viovu.

**40.Mheshmiwa Spika,** Wizara kupitia Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni imefanikiwa kuhakiki na kukagua kazi za Sanaa ya maonesho **137** kwa lengo la kuzihakiki na kuzitoa

makosa ya kimaadili ili ziweze kutumika hadharani. Aidha, Baraza la Sanaa limesajili upya vikundi **256** vya Sanaa na Utamaduni kwa lengo la kuviwezesha kufanya kazi zake kwa mujibu ya Sheria ya Baraza la Sanaa Nam 7 ya Mwaka 2015.

**41.Mheshimiwa Spika,** Jumla ya taasisi **201** zinazo jishughulisha na sanaa na burdani zimefanyiwa ukaguzi ili kuhakikisha kwamba katika taasisi hizo shughuli za burudani zinafanyika kwa mujibu wa Sheria na kuzingatia mila, silka, desturi na utamaduni wa Mzanzibari. Maeneo yaliyofanyiwa ukaguzi ni hoteli **121,** Baa **41** na Kumbi za Muziki **39**. Aidha, Wizara kupitia Baraza la Sanaa imetoa Tuzo kwa wasanii wakonge wa Zanzibar wakiwemo Prof. Mohammed Ilyas, Ndg: Iddi Suwed na Bi Njiwa. Pia, Wizara imetoa tuzo kwa kikundi cha ***Culture Musical Club na Malindi Nad Ahwani Swafaa*** Ikiwa ni ishara ya kuthamini na kuenzi kazi zao zilizoijengea heshima kubwa nchi yetu.

**42.Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Baraza la Kiswahili la Zanzibar limefanikiwa kutoa mafunzo ya ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni kwa washiriki 49 (wanaume 20 na wanawake 29) kutoka taasisi mbali mbali za elimu. Mafunzo hayo yaliendeshwa kwa muda wa siku tano kuanzia tarehe 26 hadi 30 Agosti 2024. Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wa mbinu za ufundishaji wa Kiswahili ili waweze kuzifikia na kuzitumia fursa za kukibidhaisha Kiswahili kwa kusomesha wageni ndani na nje ya nchi.

**43.Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Baraza la Kiswahili la Zanzibar limefanikiwa kutoa elimu juu ya kuimarisha na kuendeleza matumizi fasaha na sanifu ya lugha ya Kiswahili ndani na nje ya Zanzibar. Elimu hiyo imetolewa kupitia vyombo vya habari kama vile ZBC, TBC, Sauti ya America na Redio UN. Mada zilizojadiliwa ni pamoja na Kiswahili na Maendeleo ya Teknolojia, Nafasi ya Riwaya katika zama za kidijitali, Nafasi ya Mwanamke katika Uongozi, Changamoto za Lugha ya Kiswahili na namna ya kuzitatua na mchango wa Vijana katika maendeleo ya Kiswahili.

**44.Mheshimiwa Spika,** Baraza limefanikiwa kuhariri na kufanya mapitio ya mwongozo wa Literacy and Numeracy Frame Work kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar,

mwongozo wa Uthamini wa Mali na Malipo ya Fidia ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi Zanzibar, kitabu kiitwacho Safari ya Kustaafu na kitabu cha Biashara yenye Mafanikio na kutafsiri Sera ya Taifa ya Makumbusho kutoka Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale.

**45.Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Baraza imefanikiwa kuandaa Kongamano la Nane la Kiswahili la Kimataifa lilowashirikisha takriban watu 300 kutoka nchi mbali mbali duniani kama vile Canada, Marekani, China, Jamhuri ya Demokrasia ya Congo, Uganda, Kenya, Comoro, na wenyeji wa Tanzania Bara na Zanzibar. Mada kuu ya Kongamano hilo ilikuwa ni Kiswahili katika ***Miongo Tisa ya Usanifishaji*** na shabaha yake ni ***Kutathmini Maendeleo ya Kiswahili katika Miongo tisa ya Usanifishaji***. Lengo kuu la Kongamano hilo ni kutoa fursa pana kwa washiriki kujadili masuala mbalimbali ya Kiswahili hususani Maendeleo ya Kiswahili katika Miongo Tisa ya Usanifishaji. Shughuli kuu zilizofanyika ni uwasilishaji wa Makala elekezi, uwasilishaji wa Makala za mada ndogo ndogo, uzinduzi wa matokeo ya Utafiti wa msamiati wa Viumbe Bahari na mazingira yao, maonesho ya wajasiriamali wa bidhaa mbalimbali za kiutamaduni vikiwemo vitabu, usiku wa mswahili na ziara ya kutembelea vivutio mbali mbali vya kiutalii.

**46.Mheshimiwa Spika,** Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Japan International Coorporation Agency (JICA) limefanikiwa kuandaa mashindano ya Riadha ya wanawake kwanza (ladies first) yaliofanyika katika viwanja vya New Amaan Complex. Mashindano haya ni mara ya kwanza kufanyika hapa nchini tangu yalipoanzishwa Tanzania mwaka 2018. Jumla ya wanariadha 50 wa kike chini ya miaka 20 kutoka mikoa yote ya Zanzibar walishiriki katika mashindano. Na Mkoa wa Mjini Magharibi ulipata nafasi ya kwanza katika mashindano hayo.

**47.Mheshimiwa Spika,** katika kukuza na kuimarisha Michezo, Serikali kupitia Idara ya Michezo na Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar kwa kushirikiana na chama cha vishada imefanikisha mashindano ya mchezo wa vishada vya baharini (KITESURFING) ya kimataifa yaliyofanyika tarehe 24 Febuari, 2025 huko Kiwengwa. Mashindano hayo yalifanyika kwa mara ya tatu hapa Zanzibar na

kushirikisha wacheza vishada kutoka Tanzania bara, Zanzibar, Hispania, Italia, Afrika ya Kusini, Urusi, Jamhuri ya watu wa cheki na Ufaransa. Mshindi wa mashindano hayo alikuwa ni kijana kutoka Zanzibar ambae alijinyakulia zawadi ya **Dola za Kimarekani 3,000.**

**48.Mheshimiwa Spika,** katika kukuza nakuimarisha Michezo, Serikali imeziwezesha timu za Taifa kushiriki mashindano ya kikanda na kimataifa pamoja na chama cha Karate kushiriki katika mashindano ya kikanda yaliyofanyika nchini Congo tarehe 6/10/2024, sambamba na kusaidia chama cha mchezo wa Baseball kushiriki mashindano ya Baseball yaliyofanyika tarehe 27/28/2024 nchini Kenya pamoja na safari ya wachezaji kutoka Zanzibar wa Timu ya Taifa ya Tanzania ya mchezo wa kuogelea kwa watu wenye ulemavu uliofanyika tarehe 14/10/2024 Gymkhana jijini Dar es salaam.

**49.Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuyaunga mkono Mashirikisho ya mchezo wa mpira wa kikapu Zanzibar na Tanzania Bara katika kufanikisha kuandaa ligi ya mchezo wa mpira wa kikapu kwa vilabu vya wanawake kwa ukanda wa tano wa Afrika yaliyofanyika Oktoba 27 hadi Novemba 2, 2024 katika ukumbi wa michezo ya ndani wa New Amaan Complex. Washindi wa jumla katika mashindano hayo ni timu ya wanawake ya Al-Ahly kutoka Misri. Sambamba na hilo, Serikali ilisaidia chama cha TAEKWONDO kuandaa mashindano ya sita ya TAEKWONDO ya Afrika Mashariki yaliyofanyika tarehe 23 hadi 25 Agosti, 2025 katika ukumbi wa mchezo wa Judo wa Amaan Complex. Mashindano hayo yalishirikisha nchi mbali mbali zikiwemo Zanzibar, Tanzania bara, Kenya, Uganda, Zimbabwe na Ethopia ambapo mshindi wa kwanza ni kijana kutoka Zanzibar.

**50.Mheshimiwa Spika,** naomba niseme kwamba Mashindano haya ya michezo mitatu (RIADHA, MPIRA WA KIKAPU na TAEKWONDO) yaliyochezwa katika ngazi ya Kimataifa yamefanyika kwa mara ya kwanza hapa Zanzibar baada ya ujenzi wa viwanja vyetu vipya vya New Amaan Complex.

**51.Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Baraza la michezo Zanzibar kwa kushirikiana na chama cha watunisha misuli Zanzibar imefanikiwa kuandaa mashindano makubwa ya mchezo wa kutunisha misuli (body building) yaliofanyika mwezi septemba, 2024 katika ukumbi wa Ngome Kongwe na yalijulikana kwa jina la Mr: Zanzibar. Kwa kipindi kirefu mashindano hayo yalikuwa hayajafanyika hapa Zanzibar. Kufanyika kwa mashindano haya yaliibua hamasa kubwa kwa vijana na mashabiki wa mchezo huo. Mshindi wa kwanza wa mashindano hayo ni kijana kutoka Zanzibar ambaye alipata fursa ya kushiriki mashindano mengine ya kutunisha misuli yaliofanyika Kenya na Jamaica.

**52.Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyengine, Chama Cha Netball cha Zanzibar na Tanzania Bara vimelipiwa ada ya mwaka ya uwanachama ili viweze kuendelea kutambulika Kikanda na Kimataifa. Chama cha Trithlon kimewezeshwa kushiriki uchaguzi mkuu wa dunia wa Trithlon tarehe 18-21 Novemba 2024 nchini Hispania. Aidha, Chama cha Mchezo wa mazoezi ya viungo (ZABESA) kimewezeshwa kufanya mkutano mkuu wa chama hicho uliofanyika hapa Zanzibar 2024.

**53.Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuratibu mashindano makubwa ya Kombe la Mapinduzi ambapo kwa msimu wa mwaka 2024/2025 yalishirikisha timu za Taifa kutoka Bokinafaso, Kenya, Tanzania Bara na wenyeji Zanzibar. Timu ya Taifa ya Zanzibar iliibuka kidedea katika mashindano hayo. Vile vile, Wizara imefanikisha kufanyika kwa Tamasha la mazoezi ya viungo Kitaifa hapa Zanzibar ambalo hufanyika tarehe 01 Januari, ya kila mwaka. Kwa mwaka 2025 jumla ya vilabu **102** vilishiriki, vikiwemo vilabu kutoka Unguja, vilabu 35 kutoka Pemba, vilabu **10** kutoka Tanzania Bara na zaidi ya wanamazoezi **2,700** walishiriki.

**Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

**54.Mheshimiwa Spika,** kupitia Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Wizara imetekeleza Miradi ifuatayo:-

**a.Mradi wa Ujenzi wa Viwanja vya Mikoa na Wilaya**

**55.Mheshimiwa Spika,** Mradi wa ujenzi wa viwanja vya Mikoa na Wilaya unahusisha ujenzi wa viwanja 17 ambavyo vinajengwa katika Mkoa na Wilaya za Zanzibar likiwemo na eneo la michezo la Maisara (Maisara Complex). Mradi utagharimu jumla ya **TZS bilioni 132.8** kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha, Mradi unatekelezwa na Mkandarasi Reform Sports na kusimamiwa na Mshauri elekezi AE & Q Consultant co.ltd. Kupitia utekelezaji wa mradi huu, Mkandarasi atalipwa kwa awamu kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2024/2025 hadi 2028/2029.

**56.Mheshimiwa Spika,** viwanja ambavyo vimeanza kujengwa ni eneo la michezo la Maisara (92%), Kilimani (100%), Kitope (100%), Kitogani (15%), Mao ze Dong (100%), Gombani (100%), Kangani (15%) na Kishindeni (15%). Aidha, utekelezaji wa mradi kwa ujumla umefikia 32%. Maeneo ambayo bado hayajaanza utekelezaji ni Mwehe, Unguja Ukuu, Mombasa, Maruhubi, Kama, Pangatupu, Mkokotoni, Ukutini, Pandani na Micheweni.

**b.Ukarabati wa uwanja wa Gombani**

**57.Mheshimiwa Spika,** Mradi wa ukarabati wa uwanja wa Gombani awamu ya pili umetekelezwa kwa fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mradi huu umetekelezwa na Kampuni ya Ujenzi ya Reform Spots ya nchini Uturuki na kusimamiwa na Mshauri Elekezi Wakala wa Majengo Zanzibar. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa paa katika eneo la mzunguko, uwekaji wa viti vya watazamaji, ukarabati wa vyumba vya kubadilishia nguo wachezaji, ujenzi wa uzio, ujenzi wa eneo la kuegesha magari, ukarabati wa eneo la watu mashuhuri, ukarabati wa vyumba vya watu mashuhuri, na ukarabati wa vyoo na mifumo ya maji taka. Hadi kufikia Machi, 2025 Mradi wa ukarabati wa uwanja wa Gombani umefikia asilimia **98.**

**c.Ukarabati wa Uwanja wa Amaan**

**58.Mhesimiwa Spika,** ukarabati wa uwanja wa Amaan awamu ya pili ulitokana na mapendekezo ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF) ili kuufanya uwanja kukidhi vigezo vya FIFA/CAF. Mkandarasi wa ujenzi ni Kampuni ya Orkun Group na mshauri

elekezi ni Wakala wa Majengo Zanzibar. Shughuli zilizotekelezwa katika mradi huo ni pamoja na kuiongezea hadhi hotel ya Amaan kuwa ya nyota nne (4), kubadilisha nyasi bandia na kuweka nyasi asili (hybrid) kwa viwanja vyote vitatu (3) na ubadilishaji wa taa zote kwa uwanja mkubwa. Mradi tayari umekamilika kwa asilimia **100** na upo katika kipindi cha uangalizi.

**d.Mradi wa Michezo kwa Maendeleo Afrika**

**59.Mheshimiwa Spika,** mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano na Washirika wa Maendeleo (Shirika la Kimataifa la Ujerumani GIZ). Mradi umegharimu **TZS bilioni 1.98** na hadi kufikia Machi 2025 jumla ya **TZS bilioni 1.14** sawa na asilimia **57.6** zimelipwa.

**60.Mheshimiwa Spika,** kupitia mradi huu jumla ya viwanja 6 vya michezo ya mpira wa mikono vimejengwa ambapo kila kiwanja kimoja kina uwezo wa kuchezewa michezo minne ambayo ni Basketball, Netball, Vallyball na Tenis kwa nyakati tofauti. Maeneo yanayotekelezwa mradi ni Tumbatu, Mkokotoni na Rege za Mwendo kwa upande wa Unguja; Kangani, Mchangamdogo na Tennis (Chake Chake) kwa upande wa Pemba. Mradi unatarajiwa kukamilika Mei, 2025, ambapo kwa sasa utekelezaji kwa ujumla umefikia asilimia **95.**

**e.Mradi wa Ujenzi wa Nyumba ya Sanaa**

**61.Mheshimiwa Spika,** Mradi wa ujenzi wa Nyumba ya Sanaa unatekelezwa kupitia programu ya Maendeleo ya Utamaduni na Michezo kwa fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mradi unagharimu jumla ya shilingi bilioni 3.696 na hadi kufikia Machi, 2025 shilingi bilioni 1.22 zimelipwa kwa mkandarasi sawa na asilimia 33.1. Mradi unajumuisha ujenzi wa jengo lenye ghorofa tatu (G+3) na ununuzi wa samani na vifaa vya ofisi. Hatua ya utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 87.

**Programu ya Uendeshaji na Mipango Katika Sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo**

**62.Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa 2024/2025 programu hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 4,017,802,000** kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya s**hilingi bilioni 2,300,849,735/-** sawa na asilimia **57** imepatikana. ***Kiambatisho Nambari kinahusika***

**63.Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kuimarisha mazingira bora ya kazi kwa kuwapatia wafanyakazi vitendea kazi na vifaa mbali mbali vya kazi kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa kazi. Sambamba na hilo, Wizara imefanikiwa kulipa stahiki za wafanyakazi zikiwemo huduma ya likizo, ubani wa ufiwa, malipo ya safari kikazi na malipo baada ya saa za kazi. Aidha, Wizara inaendelea kusimamia mpango wa rasilimali watu wa miaka mitano na Mpango wa manunuzi wa mwaka 2024/2025.

**64.Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kuwawezesha watumishi wake kushiriki mafunzo mbali mbali kwa lengo la kuboresha utendaji mzuri wa kazi na kupata ufanisi. Jumla ya wafanyakazi 23 (wanaume 8 na wanawake 15) wamewezeshwa kushiriki mafunzo ya muda mrefu na wafanyakazi 17 (wanaume 5 na wanawake 12) mafunzo ya muda mfupi katika ngazi na fani tofauti. Aidha, Wizara inaendelea kusimamia nidhamu za wafanyakazi sambamba na kuwahimiza kutekeleza wajibu wao wanapokuwa kazini.

**65.Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kuratibu vikao mbalimbali vikiwemo vikao vya Kamati ya Uongozi Kamati Tendaji, bodi ya zabuni na vikao vya Kamati ya Ukaguzi ya Wizara. Lengo la vikao hivyo ni kuongeza ufanisi na kasi ya utekelezaji wa malengo ya Wizara. Aidha, kupitia kitengo cha Habari na Mawasiliano cha Wizara kimeweza kurusha hewani habari na matukio mbalimbali yanayohusu Wizara kupitia mitandao ya kijamii kama vile facebook, Instagram, Mtandao wa X, whatsapp pamoja na Website ya Wizara.

**66.Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kufanya mapitio ya Sera ya Utamaduni ya mwaka 2005, kufanya mapitio ya Sheria ya Usajili wa Magazeti, Vitabu na Mawakala wa Habari Namba 5 ya mwaka 1988 na kufanya mapitio ya sheria ya kuanzisha Magazeti ya Serikali Zanzibar nambari 11 ya mwaka 2008.Rasimu zote zipo katika hatua ya kupitiwa na Kamati ya Baraza la Mapinduzi ya Katiba na Sheria. Vile vile, Wizara kwa kushirikiana na (GIZ) imeandaa Mpango *Mkakati Jumuishi wa Jinsia katika Michezo na Muongozo wa Ulinzi na Kujenga Mazingira Salama na Jumuishi ya Michezo Zanzibar.* Lengo la miongozo hiyo ni kulinda usalama na haki za wanamichezo na kuifanya michezo kuwa jumuishi kwa jinsia zote.

**67.Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kwamba program ya miradi ya maendeleo inatekelezwa kwa ufanisi, Wizara imekuwa mstari wa mbele katika kufuatilia na kusimamia miradi Unguja na Pemba. Aidha, Wizara imeendelea kuratibu vikao na ziara za Kamati za Baraza la Wawakilishi zenye lengo la kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali. Katika hatua nyengine, maafisa wawili wa Idara ya Mipango walishiriki katika vikao tofauti vya ushirikiano vilivyofanyika Dodoma na Morogoro. Vikao hivyo vilikuwa katika ngazi ya wataalamu vilivyojadili ushirikiano baina ya Tanzania na Misri, Tanzania na UAE na Tanzania na Comoro. Lengo la vikao hivyo ni kuboresha uhusiano wa Kidiplomasia katika maeneo mbali mbali ya kiutendaji baina ya Tanzania na nchi za nje.

**68.Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu Pemba imefanikiwa kuratibu shughuli za Wizara kwa kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa program na Miradi ya Wizara kwa upande wa Pemba. Miongoni mwa shughuli zilizofuatiliwa ni Mradi wa Ukarabati wa Uwanja wa Gombani, Mradi wa Ujenzi wa Viwanja vya Mikoa na Wilaya, kuratibu na kusimamia shughuli za Habari, kusimamia shughuli za Michezo, kusimamia na kufuatilia program mbalimbali za maendeleo ya Vijana, kusimamia tamasha la Utamaduni wa Mzanzibari pamoja na kusimamia shughuli za Sanaa na wasanii kwa upande wa Pemba.

**69.Mheshimiwa Spika,** Uwezo wa wafanyakazi umeendelea kuimarika na wenye kuleta ufanisi zaidi kutokana na kuendeleza program za kujenga uwezo wao kitaaluma kwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kulingana na mahitaji. Mfanyakazi mmoja anaendelea na mafunzo ya muda mrefu katika stashahada ya Utunzaji wa kumbukumbu na wafanyakazi wanne wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi kulingana na kada zao za kazi kwa lengo la kuwaongezea ufanisi wa utendaji wao wa kazi. Aidha, wafanyakazi (2) wamepatiwa mafunzo ya awali ya namna ya ufanyaji kazi za Serikali (Induction Course).

**70.Mheshimiwa Spika,** Watendaji wa Ofisi Kuu Pemba wamefanya vikao mbalimbali vya wafanyakazi na vikao vya Kamati Tendaji kwa lengo la kuhimiza utekelezaji wa majukumu ya Serikali na kukumbushia haki na wajibu wa kila mfanyakazi. Aidha, Ofisi

kuu Pemba imefanikiwa kuratibu vikao na ziara za Kamati ya Kudumu za Baraza la Wawakilishi.

**71.Mheshimiwa Spika,** Ofisi kuu Pemba imeweza kuimarisha mazingira mazuri ya kazi kwa kuwapatia wafanyakazi huduma na vitendea kazi kama vile vyombo vya usafiri, printa, projekta, pamoja na vifaa mbali mbali kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa kiutendaji. Sambamba na hilo, wafanyakazi wamepatiwa stahiki zao kama vile malipo baada ya saa za kazi, huduma za likizo, fedha za safari kikazi, haki ya likizo na ubani wa ufiwa. Pia, ofisi inaendelea kusimamia na kuratibu shughuli za Wizara kwa upande wa Pemba na kusimamia utekelezaji wa mpango wa rasilimali watu wa miaka mitano.

**Fungu J05: Tume ya Utangazaji Zanzibar**

**72.Muheshimiwa Spika,** Fungu J05 linahusisha programu Kuu mbili ambazo ni: -

**a.Programu ya Maendeleo ya Habari na Utangazaji**

**73.Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025 programu imepangiwa kutumia **shilingi milioni 284,171,000/-** kwa Matumizi mengineyo. Hadi machi 2024, **shilingi milioni 99,941,379/-** zimepatikana sawa na asilimia **35** ya lengo. **Kiambatanisho nambari 1A kinahusika**

**74.Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa kazi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ni kama ifuatavyo: -

i. Leseni za utangazaji zimetolewa kwa vituo 15 vya kurushia Matangazo vikiwemo TV, Redio na TV za mtandaoni;

ii. Ukaguzi wa vituo vya utangazaji 50 umefanyika kwa ajili ya kutathmini utendaji wa kazi kulingana na masharti ya leseni zilizotolewa. Aidha, Tume imefuatilia maudhui ya vituo 27 vya redio ili kuhakikisha vituo hivyo vinafuata maadili na masharti ya leseni za utangazaji;

iii. Tume ya Utangazaji imeandaa Kanuni za Huduma za Utangazaji wakati wa Uchaguzi na kwa sasa ipo katika hatu za mwisho;

iv. Vikao 2 vya ushirikiano kati ya Tume ya Utangazaji Zanzibar na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) vimefanyika. Vikao hivyo vimejadili namna ya kuingiza teknolojia mpya ya Utangazaji wa sauti (Digital Sound Broadcasting), malipo ya vifurushi vya huduma ya utangazaji wa televisheni kwa kituo cha Azam Media na namna ya kuongeza usikivu wa vituo vya redio za FM baina ya Tanzania Bara na Zanzibar.

**b.Programu ya Utumishi na Uendeshaji**

**75.Muheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 programu imepangiwa kutumia **shilingi bilioni 1,200,029,000/- (Mishahara Shilingi milioni 837,200,000/-** na Matumizi mengineyo **Shilingi milioni 362,829,000/-).** Hadi machi 2025, **shilingi milioni 628,771,735/-** zimepatikana sawa na asilimia **52** ya lengo. Kati ya fedha hizo **shilingi milioni 530,651,314/-** sawa na asilimia **63** zimetumika kwa mishahara na **shilingi milioni 98,120,421/-** sawa na asilimia **27** zimetumika kwa Matumizi Mengineyo. **Kiambatanisho nambari 1A kinahusika.**

**76.Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa kazi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ni kama ifuatavyo: -

i. Jumla ya Wafanyakazi 37 wa Tume ya Utangazaji wamepatiwa stahiki zao sambamba na upatikanaji wa huduma za utawala na uendeshaji wa ofisi kwa lengo la kuongeza ufanisi na kuweka mazingira bora ya kazi;

ii. Wafanyakazi wawili wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu ngazi ya Shahada ya kwanza katika fani ya Teknolojia ya Mawasiliano na Biashara na Stashahada katika fani ya Uongozi wa Biashara (Chuo cha Zanzibar University); na

iii. Vikao 3 vya Bodi ya Tume ya Utangazaji vimefanyika na kujadili mambo mbali mbali ikiwemo leseni za vituo vya utangazaji na namna ya kusimamia na kutoa miongozo kwa vituo vya utangazaji;

iv. Vikao 2 vya wafanyakazi wa Tume ya Utangazaji vimefanyika kwa lengo la kusikiliza matatizo yanayowakabili na kuwapatia miongozo na maelekezo kwa mujibu wa sheria na Kanuni za Kiutumishi.

## E. MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**77.Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2025/2026, imezingatia mpango mkakati wa Wizara 2023-2026, Sera za Wizara, Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021/2026, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020/2050 na Ilani ya CCM 2020/2025.

### Vipaombele vya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2025/2026

**78.Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo imepanga kutekeleza bajeti kwa kuzingatia vipaombele vifuatavyo:-

i. Kusimamia masuala ya habari na utangazaji kwa kuzijengea uwezo Idara ya habari maelezo na tume ya utangazaji;

ii. Kuimarisha Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) na Kampuni ya ZMUX kwa kuzipatia vifaa, wataalamu na miundombinu imara ya kurushia matangazo ili viweze kutayarisha na kurusha hewani vipindi vyenye ubora;

iii. Kuimarisha uwezo wa Shirika la Magazeti ya Serikali kwa kuijengea ofisi na Kiwanda cha kuchapicha magazeti kwa lengo la kupunguza gharama za uchapishaji wa magazeti;

iv. Kuthibiti na kusimamia waandishi wa habari wanaofanya kazi ndani na nje ya Zanzibar pamoja na kusimamia Sera na sheria za habari na maadili ya waandishi wa habari;

v. Kutoa huduma za Bohari kuu ya vifaa vya ofisi na kuandikia kwa Taasisi za Serikali na Binafsi;

vi. Kuratibu na kusimamia shughuli za maendeleo ya vijana nchini na kuwawezesha vijana kwa kuwajengea uwezo ili kuimarika kiuchumi, kijamii na kisiasa;

vii. Kuimarisha Mabaraza ya Vijana kiutendaji na kuhamasisha ushiriki na ushirikishwaji wa vijana katika fursa mbali mbali kupitia ngazi za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa;

viii. Kutoa elimu kwa jamii juu ya kulinda mila silka na utamaduni wa mzanzibari na kuwajengea uwezo wajasiriamali wa

bidhaa za kiutamaduni;

ix. Kusimamia shughuli za sanaa na Burudani pamoja na kuwaunganisha wasanii na fursa mbali mbali ndani na nje ya nchi;

x. Kuendeleza, kukuza na kueneza matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu kwa wageni na wenyeji pamoja na kutoa mafunzo ya mbinu za kufundisha Kiswahili;

xi. Kusimamia na kuimarisha miondombinu ya michezo pamoja na kuratibu maendeleo ya michezo kwa kuviwezesha vyama vya michezo kuendesha shughuli zao kwa mujibu wa Sera na Sheria;

xii. Kukamilisha Sera, Sheria na Kanuni za Wizara ambazo zimefanyiwa mapitio ili ziweze kutumika, kufanya ufuatiliaji wa miradi na program pamoja na kufanya tafiti katika Sekta ya Habari Vijana Utamadini na Michezo; na

xiii. Kuimarisha mazingira mazuri ya utendaji kazi na wafanyakazi ikiwemo utoaji wa vitendea kazi na stahiki za wafanyakazi kwa mujibu wa sheria na kuwaendeleza kwa kuwapatia mafunzo.

**79.Mheshimiwa Spika,** Wizara Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo inatekekeza bajeti yake kupitia mafungu ya bajeti 2 na Programu kuu 4. Malengo ya Utekelezaji kwa kila fungu la bajeti na Programu kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ni kama inavyowasilishwa hapo chini:-

**Fungu J03: Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo**

**80.Mheshimiwa spika;** Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo inasimamia programu kuu nne na programu ndogo nane kama zifutazo;-

**A.Programu ya Maendeleo ya Habari, Utangazaji na Uchapaji**

**81.Mheshimiwa Spika,** Programu hii itakuwa na programu ndogo mbili ambazo ni Upatikanaji na Usambazaji wa Habari na Usimamizi wa vyombo vya habari, Utangazaji na Uchapaji. Katika kulifikia lengo la programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kuimarisha utoaji wa huduma taarifa za Serikali, picha na filamu za kisasa;

ii. Kutoa huduma za uchapaji kwa taasisi za Serikali na Binafsi;

iii. Kuendeleza biashara ya vingamuzi pamoja na maudhui yenye mvuto kwa lengo la kuelimisha;

iv. Kutoa huduma za Bohari kuu ya vifaa vya ofisi na kuandikia kwa Taasisi za Serikali na Binafsi;

v. Kutoa taarifa na matukio sahihi na yanayoaminika kwa jamii na kwa wakati;

vi. Kuendesha, kusimamia na kuchapisha gazeti la Serikali;

vii. Kutoa/kusambaza taarifa, habari na sera za Serikali kwa umma; na

viii. Kuendelea Kuzalisha vipindi bora vyenye maadili na nidhamu vinavyoendana na mahitaji ya Wazanzibari.

**82.Mheshimiwa Spika,** ili programu ya Maendeleo ya Habari, Utangazaji na Uchapaji miweze kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ninaliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi bilioni 9,167,152,000/-** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. **Kiambatanisho nambari 1F na 1G kinahusika.**

**B. Programu Kuu ya Maendeleo ya Vijana**

**83.Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Programu hii itakuwa na programu ndogo moja ambayo ni Programu ya Maendeleo ya Vijana. Katika kufikia malengo ya programu shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kuandaa, kusimamia na kuratibu utekelezaji wa sera, sheria, mipango na programu za maendeleo ya vijana nchini;

ii. Kuratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa;

iii. Kuimarisha ushiriki na ushirikishwaji wa vijana katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii;

iv. Kutekeleza programu za elimu na malezi kwa vijana pamoja na mikakati ya kujenga moyo wa Uzalendo, ari ya kujitolea na kuipenda nchi yao; na

v. Kufanya ufuatiliaji wa mabaraza ya vijana Wilaya na shehia pamoja na kuyasaidia Mabaraza ya vijana Taifa, Wilaya na Shehia.

**84.Mheshimiwa Spika,** ili programu ya Maendelo ya Vijana iweze kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2025/2026, naliomba Bazara lako tukufu kuidhinisha jumla ya **shillingi bilioni 18,260,503,000/-** kati ya hizo **shilingi bilioni 1,760,503,000/-** kwa matumizi ya kazi za kawaida na **shilingi bilioni 16,500,000,000/-** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**C. Programu Kuu ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.**

**85.Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Programu hii itakuwa na programu ndogo mbili ambazo ni Programu Ndogo ya Uimarishaji, Uhifadhi, Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa; na Programu Ndogo ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Michezo. Katika kulifikia lengo la programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kuandaa Tamasha la Utamaduni wa Mzanzibari na kuyaendeleza Matamasha ya kijamii;

ii. Kutoa elimu ya kulinda, kuhifadhi na kuendeleza mila, silka na desturi za Mzanzibari;

iii. Kuendelea na ukaguzi wa Filamu na kazi za Sanaa za maonyesho;

iv. Kutoa elimu kwa wasanii juu ya umuhimu wa kujisajili pamoja na umuhimu wa mikataba na urasimishaji wa kazi za sanaa;

v. Kutoa elimu kuhusu matumizi ya Kiswahili fasaha kwa wageni na wenyeji kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii;

vi. Kujenga na kuimarisha viwanja vya michezo Zanzibar;

vii. Kuwezesha timu za Taifa kushiriki katika mashindano ya Kikanda na Kimataifa;

viii. Kuwawezesha viongozi wa vyama vya michezo, waamuzi na makocha kushiriki mafunzo ya Kikanda na Kimataifa; na

ix. Kusaidia kuandaa mashindano ya Kikanda na Kimataifa.

**86.Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026 ili Programu Kuu ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo iweze kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2025/2026, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi bilioni 421,833,856,000/-** kati ya hizo **shilingi bilioni 4,749,874,000/- kwa matumizi ya kazi za kawaida na shilingi bilioni 417,083,982,000/-** kwa matumizi ya miradi ya Maendeleo.

### D.Progromu Kuu ya Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo

**87.Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Programu hii itakuwa na programu ndogo tatu ambazo Programu Ndogo ya Uratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara; Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na Programu Ndogo ya Uratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba. Katika kulifikia lengo la programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kuwaendeleza wafanyakazi kitaaluma kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu;

ii. Kuimarisha mazingira bora ya kazi kwa kuwapatia wafanyakazi vifaa vya ofisi na huduma;

iii. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Wizara Ofisi Kuu Pemba;

iv. Kuratibu na kusimamia mipango, sera na tafiti za Wizara; na

v. Kuratibu, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa programu za miradi na shughuli za Wizara.

**88.Mheshimiwa Spika,** ili programu Kuu ya Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo iweze kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2025/2026, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya shilingi bilioni 4,129,582,000/- kwa matumizi ya kazi za kawaida.

**Fungu J05: Tume ya Utangazaji Zanzibar**

**89.Mheshimiwa spika;** Tume ya Utangazaji Zanazibar inasimamia programu kuu mbili na programu ndogo tatu kama zifutazo;-

**A.Programu Kuu ya Maendeleo ya Habari na Utangazaji**

**90.Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Programu hii itakuwa na programu ndogo moja ambayo ni Usimamizi wa vyombo vya Utangazaji. Katika kulifikia lengo la programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kufanya ufuatiliaji wa maudhui wa vituo vya utangazaji;

ii. Kusimamia masafa ya utangazaji

iii. Kuandaa kanuni na miongozo ya utangazaji

iv. Kuandaa na kufanya kongamano la mwaka

**91.Mheshimiwa Spika,** ili programu Kuu ya Maendeleo ya Habari na Utangazaji iweze kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2025/2026, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **shilingi milioni 172,018,000/-** kwa matumizi ya kazi za kawaida.

**B.Programu kuu ya Utumishi na Uendeshaji**

**92.Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Programu hii itakuwa na programu ndogo mbili ambazo ni Usimamizi wa rasilimali watu na Utawala na Uendeshaji. Katika kulifikia lengo la programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa;-

i. Kuwajengea uwezo watendaji wa tume ya utangazaji,

ii. Kulipa stahiki za wafanyakazi,

iii. Kuweka mazingira mazuri ya ofisi kwa kuipa vifaa na huduma muhimu na,

iv. Kuitangaza Tume ya Utangazaji Zanzibar kwa umma.

**93.Mheshimiwa Spika,** ili programu Kuu ya Utumishi na Uendeshaji iweze kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2025/2026, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi bilioni 1,284,882,000/-** kwa matumizi ya kazi za kawaida.

## F. MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

***FUNGU J03: Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo***

**94.Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kutekeleza kazi zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha makadirio ya matumizi ya Programu zenye jumla ya **shilingi bilioni 453,391,093,000/-.** Kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 19,807,111,000** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida na **shilingi bilioni 433,583,982,000/-** kwa miradi ya maendeleo. Aidha, fedha za miradi ya maendeleo **shilingi bilioni**

**432,950,000,000/-** kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na **shilingi milioni 633,982,000/-** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. **Kiambatisho nambari 1F na 1G kinahusika.**

***FUNGU J05: Tume ya Utangazaji Zanzibar***

**95.Mheshimiwa Spika** ili kuiwezesha Tume ya Utangazaji Zanzibar kutekeleza kazi zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026, ninaliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha makadirio ya matumizi ya Programu zenye jumla ya **shilingi bilioni 1,456,900,000/-** kwa matumizi ya kazi za kawaida. **Kiambatisho nambari 1F na 1G kinahusika.**

**96. Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha ukusanyaji wa mapato yanayotokana na vyanzo mbalimbali yenye jumla ya **shilingi 710,017,000/-** ikiwa ni makusanyo ya fedha zinazoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Mgawanyo wa fedha za makusanyo hayo umeainishwa kwenye **Kiambatisho nambari 1H.**

## G. MWISHO

**97.Mheshimiwa Spika,** kwa mara nyengine tena, nakushkuru wewe binafsi Naibu Spika, Waheshimiwa Mawaziri,na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa ushirikiano wenu mkubwa mnaoendelea kuipatia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Nidhahiri kwamba mafanikio ya utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara hii yameweza kupatikana kutokana na ushirikiano wenu.

**98.Mheshimiwa Spika,** nawashukuru na kuwapongeza kwa dhati watendaji wangu wote wakiongozwa na Katibu Mkuu, Afisa Mdhamini, Wakurugenzi, Makamishna, Makatibu Watendaji pamoja na maafisa kwa utendaji wao mzuri wa kazi ambao unarahisisha kazi zangu za uwaziri na kusimamia Wizara.

**99.Mheshimiwa Spika,** kwa umuhimu mkubwa naomba kuishukuru kwa dhati Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo ya Tanzania kwa ushirikiano makubwa ya kiutendaji

tunayoyapata katika utekelezaji wa majukumu ya kazi zetu. Vile vile ninazishukuru nchi na Mashirika ya kimaendeleo ikiwemo, Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, India, Rwanda, Shirika la Idadi ya Watu na Maendeleo (UNFPA), UNICEF,UNDP,Ubalozi wa SWETZERLAND, SAVE THE CHILDREN, ASA, UNESCO, PBZ, CRDB, NMB, Equity Bank, NIC, BANDARI, ZURA, SUZA, AZAM Media, Coaches Across Continents, Youth Challenge International, TAMWA, JUWAHAZA, TAHA, S.O.S, USAID, IRI, NDI, Restless Development, T-MARC Tanzania, Zanzibar Maisha Bora Foundation, Zanzibar Milele Foundation, Action Aid, PIRO, Feed the Future, Benki ya Tanzania, Jukwaa la Wahariri, Baraza la Habari, Asasi za Kiraia zinazosaidia vijana pamoja na Washirika wote wa Maendeleo tulioshirikiana nao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

**100.Mheshimiwa Spika,** naiomba Kamati yako ipokee, ijadili, na kupitisha bajeti hii pamoja na kutupatia ushauri na maelekezo ambayo yataimarisha utekelezaji wake.

**101.Mheshimiwa Mwenyekiti naomba kutoa hoja.**



**Mheshimiwa Tabia Maulid Mwita (MBM),**
**Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo**
**Zanzibar.**

## KIAMBATISHO NAMBA 1 A

**FEDHA ZILIZOINGIZWA KUANZIA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 KWA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU**

| NO | IDARA | MAELEZO | BAJETI 2024/2025 | FEDHA ZILIZOPATIKANA JULY -MARCH 2024/2025 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Afisi Kuu Pemba | Mishahara | 848,128,000 | 680,717,106 | 80% |
| | | Matumizi Mengineo | 295,000,000 | 189,146,250 | 64% |
| | **JUMLA** | | **1,143,128,000** | **869,863,356** | **76%** |
| 2 | Mipango, Sera na Utafiti | Mishahara | - | - | - |
| | | Matumizi Mengineo | 220,000,000 | 53,000,000 | 24% |
| | **JUMLA** | | **220,000,000** | **53,000,000** | **24%** |
| 3 | Uendeshaji na Utumishi | Mishahara | 1,811,074,000 | 1,033,896,671 | 57% |
| | | Matumizi Mengineo | 843,600,000 | 344,089,708 | 41% |
| | **JUMLA** | | **2,654,674,000** | **1,377,986,379** | **52%** |
| 4 | Maendeleo ya Vijana | Mishahara | 498,264,000 | 355,643,240 | 71% |
| | | Matumizi Mengineo | 278,850,000 | 93,100,000 | 33% |
| | **JUMLA** | | **777,114,000** | **448,743,240** | **58%** |
| 5 | Idara ya Utamaduni na Sanaa | Mishahara | 2,255,928,000 | 1,731,217,649 | 77% |
| | | Matumizi Mengineo | 310,000,000 | 64,500,000 | 21% |
| | **JUMLA** | | **2,565,928,000** | **1,795,717,649** | **70%** |
| 6 | Idara ya Michezo | Mishahara | - | - | - |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Matumizi Mengineo | 350,050,000 | 546,500,000 | 156% |
| | **JUMLA** | | **350,050,000** | **546,500,000** | **156%** |
| 7 | Idara ya Habari Maelezo | Mishahara | 543,606,000 | 503,105,085 | 93% |
| | | Matumizi Mengineo | 420,000,000 | 42,000,000 | 10% |
| | **JUMLA** | | **963,606,000** | **545,105,085** | **57%** |
| | **Jumla ya Mishahara** | | **5,957,000,000** | **4,304,579,751** | **72%** |
| | **Jumla ya Matumizi Mengine** | | **2,717,500,000** | **1,332,335,968** | **49%** |
| | **Jumla Kuu kwa Taasisi zisizopokea Ruzuku** | | **8,674,500,000** | **5,636,915,710** | **65%** |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | **TAASISI ZA RUZUKU** | | | | |
| | | | | | |
| 1 | Baraza la Vijana Zanzibar | Mishahara | - | - | - |
| | | Matumizi Mengineo | 295,600,000 | 113,044,177 | 38% |
| | | | **295,600,000** | **113,044,177** | **38%** |
| 3 | Baraza la Kiswahili Zanzibar | Mishahara | - | - | - |
| | | Matumizi Mengineo | 255,000,000 | 87,942,500 | 34% |
| | **JUMLA** | | **255,000,000** | **87,942,500** | **34%** |
| 4 | Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni Zanzibar | Mishahara | - | - | - |
| | | Matumizi Mengineo | 205,700,000 | 56,802,168 | 28% |
| | **JUMLA** | | **205,700,000** | **56,802,168** | **28%** |
| 5 | Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar | Mishahara | - | - | - |
| | | Matumizi Mengineo | 206,200,000 | 60,053,000 | 29% |
| | **JUMLA** | | **206,200,000** | **60,053,000** | **29%** |
| 6 | Tume ya Utangazaji | Mishahara | 837,200,000 | 530,651,314 | 63% |
| | | Matumizi Mengineo | 647,000,000 | 198,061,800 | 31% |
| | **JUMLA** | | **1,484,200,000** | **728,713,114** | **49%** |
| 7 | Shirika la Utangazaji (ZBC) | Mishahara | 3,763,000,000 | 2,586,765,363 | 69% |
| | | Matumizi Mengineo | 2,005,900,000 | 453,625,000 | 23% |
| | **JUMLA** | | **5,768,900,000** | **3,040,390,363** | **53%** |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 8 | Shirika la Magazeti | Mishahara | 1,276,100,000 | 912,511,360 | 72% |
| | | Matumizi Mengineo | - | - | |
| | **JUMLA** | | **1,276, 100,000** | **912,511,360** | **72%** |
| 9 | kampuni ya Uunganisha Maudhui (ZMUX) | Mishahara | - | - | - |
| | | Matumizi Mengineo | | | |
| | **JUMLA** | | | | |
| 10 | Wakala wa Serikali wa Uchapaji (ZGP) | Mishahara | 2,385,950,000 | 1,673,175,463 | 70% |
| | | Matumizi Mengineo | - | - | - |
| | **JUMLA** | | 2,385,950,000 | 1,673,175,463 | **70%** |
| | **Jumla ya Mishahara ya Ruzuku** | | **8,262,250,000** | **5,703,103,501** | **69%** |
| | **Jumla ya matumizi mengineo ya ruzuku** | | **3,615,400,000** | **969,528,645** | **27%** |
| | **JUMLA KUU YA RUZUKU** | | **11,877,650,000** | **6,672,632,146** | **56%** |
| | **Jumla ya Mishahara kwa Wizara** | | **14,219,250,000** | **10,007,683,252** | **70%** |
| | **Jumla ya matumizi mengineo ya Wizara** | | **6,332,900,000** | **2,301,864,613** | **36%** |
| | **JUMLA KUU YA WIZARA MATUMIZI YA KAWAIDA (A)** | | **20,552,150,000** | **12,309,547,865** | **60%** |
| | **Miradi ya Maendeleo** | | | | |
| 1 | Ushirikishwaji wa Vijana katika uongozi | | 90,000,000 | - | 0% |
| 2 | Ujenzi wa vituo vya Maendeleo ya vijana | | 4,500,000,000 | - | 0% |
| 3 | Ujenzi wa Viwanja vya Michezo vya Wilaya | | 60,000,000,000 | 69,782,825,084 | 116% |
| 4 | Ujkenzi wa viwanja vya michezo midogo midogo GIZ | | 633,982,000 | 1,142,566,395 | 180% |
| 5 | Ujenzi wa Nyumba ya Sanaa | | 5,000,000,000 | 1,288 073 196 | 26% |
| | **Jumla Kuu ya Wizara Miradi ya Maendeleo (B)** | | **70,223,982,000** | **72,820,017,675** | 104% |
| | **JUMLA KUU YA WIZARA (A+B)** | | **90,776,132,000** | **85,129,565,540** | **94%** |

## KIAMBATISHO NAMBA 1B

## MAPATO YALIYOKUSANYWA JULAI 2024 HADI MACHI 2025

### MAPATO YANAYOINGIA HAZINA

| NO | TAASISI | BAJETI 2024/2025 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 | ASILIMI A |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni | 270,000,000 | 224,709,250 | 83% |
| 2 | Baraza la Kiswahili Zanzibar | 40,000,000 | 7,744,500 | 19% |
| 3 | Habari Maelezo | 174,000,000 | 31,522,800 | 18% |
| 4 | Ofisi kuu Pemba | 91,000,000 | 20,015,000 | 22% |
| | **JUMLA** | **575,000,000** | **283,991,550** | **49%** |

## KIAMBATISHO NAMBA 1C

## MAPATO YANAYOTUMIWA NA TAASISI HUSIKA

| NO. | TAASISI | BAJETI 2024/2025 | MAPATO YALIYOKUSANYWA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Shirika la Utangazaji (ZBC) | 1,600,000,000 | 1,689,000,000 | 105% |
| 2 | Shirika la Magazeti (SMS) | 1,500,000,000 | 602,640,177 | 40% |
| 3 | ZGP | 7,335,168,000 | 2,617,514,260 | 36% |
| 4 | ZMUX | 1,500,000,000 | 936,197,007 | 62% |
| 5 | Tume ya Utangazaji | 362,300,000 | 228,817,800 | 63% |
| | **JUMLA** | **12,297,000,000** | **6,074,169,244** | **49%** |

## KIAMBATISHO NAMBA 1D
## FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 KWA KILA PROGRAMU NDOGO

**Programu ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa habari**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2024/2025 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Idara ya Habari Maelezo | 938,406,000 | 535,105,085 | 57% |
| 2 | Shirika la Utangazaji (ZBC) | 5,768,900,000 | 3,035,588,430 | 50% |
| 3 | Kampuni ya Usambazaji Maudhui (ZMUX) | - | - | - |
| 4 | Shirika la Magazeti ya Serikali | 1,276,100,000 | 912,511,360 | 72% |
| | **JUMLA** | **7,983,406,000** | **4,483,204,875** | **56%** |

**Programu ndogo ya Usimamizi wa Vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapishaji**

| NO | TAASISI | BAJETI 2024/2025 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| | Habari Maelezo | 25,200,000 | 10,000,000 | 40% |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Tume ya Utangazaji | 1,484,200,000 | 728,713,114 | 49% |
| | Wakala wa Serikali wa Uchapaji | 2,385,950,000 | 1,673,175,463 | 70% |
| | **JUMLA** | **3,895,350,000** | **2,411,888,577** | **62%** |

**Programu Ndogo ya Maendeleo ya Vijana**

| NO | TAASISI | BAJETI 2024/2025 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Idara ya Maendeleo ya Vijana | 777,114,000 | 448,743,240 | 58% |
| 2 | Baraza la Vijana | 295,600,000 | 113,044,177 | 38% |
| 3 | Programu ya Kuwajengea uwezo vijana | 90,000,000 | 119,530,000 | 133% |
| 4 | Ujenzi wa Vituo vya Maendeleo Vijana | 5,400,000,000 | - | 0% |
| | **Jumla** | **6,562,714,000** | **681,317,417** | **13%** |

**Programu ndogo ya Uimarishaji na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2024/2025 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Idara ya Utamaduni na Sanaa | 2,565,928,000 | 1,795,717,649 | 70% |
| 2 | Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni | 205,700,000 | 56,802,168 | 28% |
| 3 | Baraza la Kiswahili Zanzibar | 255,000,000 | 87,942,500 | 34% |
| 4 | Ujenzi wa Nyumba ya Sanaa | 5,000,000,000 | 1,288,073,196 | 26% |
| | **JUMLA** | **8,026,628,000** | **3,228,535,513** | **40%** |

**Programu ndogo ya Uendelezaji na Ukuzaji wa Michezo**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2024/2025 | FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Idara ya Michezo | 350,050,000 | 546,500,000 | 156% |
| 2 | Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar | 206,200,000 | 60,053,000 | 29% |
| 3 | Ujenzi wa Viwanja vya Michezo vya Wilaya | 60,000,000,000 | 69,782,825,084 | 116% |
| | Ujenzi wa viwanja vya michezo midogo midogo | 633,982,000 | 1,142,566,395 | 180% |
| | **JUMLA** | **61,190,232,000** | **71,531,944,479** | **117%** |

**Programu ndogo ya Uendeshaji na Usimamizi wa Sekta za Vijana, Utamaduni na Michezo**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2024/2025 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 | ASILIMI A |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Idara ya Utumishi na Uendeshaji | 2,654,674,000 | 1,377,986,379 | 52% |
| | **JUMLA** | **2,654,674,000** | **1,377,986,379** | **52%** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2024/2025 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 | ASILIMI A |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Idara ya Mipango Sera na Utafiti | 220,000,000 | 53,000,000 | 24% |
| | **JUMLA** | **220,000,000** | **53,000,000** | **24%** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2024/2025 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 | ASILIMI A |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ofisi Kuu Pemba | 1,143,128,000 | 869,863,366 | 76% |
| | **JUMLA** | **1,143,128,000** | **869,863,366** | **76%** |

## KIAMBATISHO NAMBA 1E

## FEDHA ZILIZOKUSANYWA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 KWA KILA PROGRAMU NDOGO

**Programu ndogo ya Uimarishaji na uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa**

| NO. | TAASISI | BAJETI | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 | ASILIMI A |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni | 270,000,000 | 224,709,250 | 83% |
| 2 | Baraza la Kiswahili Zanzibar | 40,000,000 | 7,744,500 | 18% |
| | **JUMLA** | **310,000,000** | **232,453,750** | **75%** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba**

| NO. | TAASISI | BAJETI | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ofisi Kuu Pemba | 91,000,000 | 20,015,000 | 22% |
| | **JUMLA** | **91,000,000** | **20,015,000** | **22%** |

## KIAMBATISHO NAMBA 1F

**BAJETI INAYOOMBWA NA WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNINA MICHEZO KWA MWAKA WA FEDHA 2(**

**TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU**

| No | IDARA | MAELEZO | BAJETI 2025/2026 |
|---|---|---|---|
| 1 | Afisi Kuu Pemba | Mishahara | 976,614,000 |
| | | Matumizi Mengineo | 400,000,000 |
| **JUMLA** | | | **1,376,614,000** |
| 2 | Mipango, Sera na Utafiti | Mishahara | - |
| | | Matumizi Mengineo | 315,800,000 |
| **JUMLA** | | | **315,800,000** |
| 3 | Uendeshaji na utumishi | Mishahara | 1,357,168,000 |
| | | Matumizi Mengineo | 1,080,000,000 |
| **JUMLA** | | | **2,437,168,000** |
| 4 | Habari Maelezo | Mishahara | 778,392,000 |
| | | Matumizi Mengineyo | 485,810,033 |
| **JUMLA** | | | **1,264,202,033** |
| 5 | Maendeleo ya Vijana | Mishahara | 594,592,000 |
| | | Matumizi Mengineo | 722,610,690 |
| **JUMLA** | | | **1,317,202,690** |
| 6 | Utamaduni na Sanaa | Mishahara | 2,448,234,000 |
| | | Matumizi Mengineo | 403,025,000 |
| **JUMLA** | | | **2,851,259,000** |
| 7 | Michezo | Mishahara | - |
| | | Matumizi Mengineo | 497,714,967 |

| | |
|---|---|
| **JUMLA** | **497,714,967** |
| **Jumla ya Mishahara** | **6,155,000,000** |
| **Jumla ya Matumizi mengine** | **3,908,511,000** |
| **Jumla Kuu kwa taasisi zisizopokea Ruzuku** | **10,063,511,000** |

**TAASISI ZA RUZUKU**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Shirika la Magazeti ya Serikali | Mishahara | 1,587,500,000 |
| | | Matumizi Mengineo | - |
| | | | **1,587,500,000** |
| 2 | Shirika la Utangazaji (ZBC) | Mishahara | 3,842,900,000 |
| | | Matumizi Mengineo | - |
| | | | **3,842,900,000** |
| 3 | Wakala wa Serikali wa Uchapaji | Mishahara | 2,475,300,000 |
| | | Matumizi Mengineo | - |
| | | | **2,475,300,000** |
| 4 | Tume ya Utangazaji | Mishahara | 777,500,000 |
| | | Matumizi Mengineo | 679,400,000 |
| | | | **1,456,900,000** |
| 5 | Kampuni ya Unganishaji Maudhui (ZMUX) | Mishahara | **-** |
| | | Matumizi Mengineo | - |
| | | | |
| 6 | Baraza la Vijana | Mishahara | - |
| | | Matumizi Mengineo | 443,300,000 |
| | **JUMLA** | | **443,300,000** |
| 7 | Baraza la Kiswahili Zanzibar | Mishahara | - |
| | | Matumizi Mengineo | 353,100,000 |
| | **JUMLA** | | **353,100,000** |
| 8 | Baraza la Sanaa,Sensa ya filamu na Utamaduni | Mishahara | - |
| | | Matumizi Mengineo | 691,000,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | **JUMLA** | | **691,000,000** |
| 9 | Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar | Mishahara | - |
| | | Matumizi Mengineo | 350,500,000 |
| | **JUMLA** | | **350,500,000** |
| | | | |
| | **Jumla ya Mishahara Ruzuku** | | **8,683,200,000** |
| | **Jumla ya matumizi mengineo ruzuku** | | **2,517,300,000** |
| | **JUMLA KUU YA RUZUKU** | | **11,200,500,000** |
| | | | |
| | **Jumla ya Mishahara kwa Wizara** | | **14,838,200,000** |
| | **Jumla ya matumizi mengineo ya Wizara** | | **6,425,811,000** |
| | **JUMLA KUU YA WIZARA (Matumizi ya kawaida) A** | | **21,264,011,000** |

| | | |
|---|---|---|
| | **MIRADI YA MAENDELEO** | |
| | Uimarishaji wa Michezo na miundombinu ya viwanja vya michezo. | 389,400,000,000 |
| | Ujenzi wa viwanja vya Wilaya na Mikoa | 40,550,000,000 |
| | Ujenzi wa wa viwanja vya michezo midogo midogo -GIZ | 633,982,000 |
| | Ujenzi wa vituo vya maendeleo ya vijana | 16,500,000,000 |
| | Ujenzi wa Nyumba ya Sanaa | 3,000,000,000 |
| | **Jumla ya Miradi ya Maendeleo B** | **433,583,982,000** |
| | **JUMLA KUU YA WIZARA ( A + B)** | **454,847,993,000** |

**KIAMBATISHO NAMBA 1G**

**BAJETI INAYOOMBWA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 KWA KILA PROGRAMU NDOGO**

**Programu Ndogo ya Maendeleo ya Vijana**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2025/2026 MATUMIZI |
|---|---|---|
| 1 | Idara ya Maendeleo Vijana | 1,317,202,690 |
| 2 | Baraza la Vijana Zanzibar | 443,300,000 |
| 3 | Ujenzi wa vituo vya maendeleo ya vijana | 16,500,000,000 |
| | **JUMLA** | **18,260,502,690** |

**Programu Ndogo ya Uimarishaji na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2025/2026 MATUMIZI |
|---|---|---|
| 1 | Idara ya Utamaduni na Sanaa na Michezo | 2,857,559,000 |
| 2 | Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni | 691,000,000 |
| 3 | Baraza la Kiswahili Zanzibar | 353,100,000 |
| 4 | Mradi wa Nyumba ya Sanaa | 3,000,000,000 |
| | **JUMLA** | **6,901,659,000** |

**Programu Ndogo ya Uendelezaji na Ukuzaji wa Michezo**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2025/2026MATUMIZI |
|---|---|---|
| 1 | Idara ya Michezo | 497,714,967 |
| 2 | Baraza la Michezo | 350,500,000 |
| 3 | Mradi wa Ujenzi wa Viwanja vidogo vidogo (GIZ) | 633,982,000 |
| 4 | Uimarishaji wa Michezo na miundombinu ya viwanja vya michezo. | 372,900,000,000 |
| 5 | Ujenzi wa viwanja vya Wilaya na Mikoa | 40,550,000,000 |
| | **JUMLA** | **414,932,196,967** |

**Programu Ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2023/2024 MATUMIZI |
|---|---|---|
| **1** | Idara ya Mipango Sera na Utafiti | 315,800,000 |
| | **JUMLA** | **315,800,000** |

**Programu Ndogo ya Uendeshaji na Usimamizi wa Sekta za Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2025/2026 MATUMIZI |
|---|---|---|
| **1** | Idara ya Utumishi na Uendeshaji | 2,437,168,000 |
| | **JUMLA** | **2,437,168,000** |

**Programu Ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2025/2026 MATUMIZI |
|---|---|---|
| 1 | Shirika la Utangazaji Zanzibar | 3,842,900,000 |
| 2 | Idara ya Habari Maelezo | 1,218,102,033 |
| 3 | Shirika la Magazeti | 1,587,500,000 |
| 5 | Kampuni ya Usambazaji wa Maudhui (ZMUX) | - |
| | **JUMLA** | **6,648,502,033** |

**Programu Ndogo ya Usimamizi wa vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapaji**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2025/2026 MATUMIZI |
|---|---|---|
| | | |
| 1 | Idara ya Habari Maelezo | 46,100,000 |
| 2 | Wakala wa Serikali wa Uchapaji | 2,475,300,000 |
| | **JUMLA** | **2,521,400,000** |

**Programu Ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2025/2026 MATUMIZI |
|---|---|---|
| | Ofisi Kuu Pemba | 1,376,614,000 |
| | **JUMLA** | **1,376,614,000** |

**Tume ya Utangazaji Zanzibar**

| NO | Programu | BAJETI 2025/2026 MATUMIZI |
|---|---|---|
| 1 | Maendeleo ya Habari na Utangazaji | 172,018,000 |
| 2 | Utumishi na Uendeshaji | 1,284,882,000 |
| | **Jumla** | **1,456,900,000** |

**KIAMBATISHI NAMBA 1H**
**MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026**

**MAPATO YANAYOINGIA HAZINA**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2025/2026 |
|---|---|---|
| 1 | Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni | 360,000,000 |
| 2 | Baraza la Kiswahili Zanzibar | 50,000,000 |

| | | |
|---|---|---|
| 3 | Habari Maelezo | 200,000,000 |
| | | |
| 4 | Ofisi Kuu Pemba | 100,017,000 |
| | **JUMLA** | **710,017,000** |

**MAPATO YATAKAYO KUSANYWA NA YANAYOTUMIWA NA TAASISI HUSIKA**

| NO | TAASISI | MAKUSANYO |
|---|---|---|
| **1** | **Shirika la Utangazaji (ZBC)** | **1,800,000,000** |
| **2** | **Shirika la Magazeti** | **1,500,000,000** |
| **3** | **ZGP** | **3,607,952,000** |
| **4** | **ZMUX** | **1,500,000,000** |
| **5** | **Tume ya Tangazaji** | **420,000,000** |

**KIAMBATANISHO NO 3C**

**MIRADI ILIYOTEMBELEWA, KUWEKWA JIWE LA MSINGI NA KUZINDULIWA NA MWENGE WA UHURU 2024 KWA KANDA YA TANO – ZANZIBAR**

| MIKOA/WILAYA | MICHANGO YA MWENGE | JUMLA YA MIRADI | MICHANGO YA WANANCHI | MICHANGO YA WILAYA | MICHANGO YA SERIKALI KUU | MICHANGO YA WAHISANI | THAMANI YA MIRADI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **KASKAZINI PEMBA** | | | | | | | |
| Micheweni | 0.00 | 8.0 | 68433000.00 | 0.00 | 3,875,623,270 | 8,945,000.00 | 3,953,001,269.69 |
| Wete | 0.00 | 7.0 | 35,000,000 | 0.00 | 1,032,583,743.02 | 20,000,000 | 1,087,583,743.02 |
| **Jumla Ndogo** | - | 15.0 | 103,433,000.0 | - | 4,908,207,012.7 | 28,945,000.0 | 5,040,585,012.7 |
| **KUSINI PEMBA** | | | | | | | |
| Chake chake | 0.00 | 8.0 | 7,350,000 | 0.00 | 9,548,141,645 | 1,094,800,000 | 10,650,291,645 |
| Mkoani | 0.00 | 9.0 | 35,789,200.00 | 0.00 | 26,196,877,498.00 | 30,500,000 | 26,263,166,698.00 |
| **Jumla Ndogo** | - | 17.0 | 43,139,200.0 | - | 35,745,019,143.0 | 1,125,300,000.0 | 36,913,458,343.0 |
| **KASKAZINI UNGUJA** | | | | | | | |
| Kaskazini Unguja A | 0.00 | 4.0 | 0.00 | 0.00 | 18,251,000,000 | 125,003,000,000.0 | 143,254,000,000.00 |
| Kaskazini Unguja B | 0.00 | 6.0 | 0.00 | 0.00 | 6,844,485,557 | 1,816,795,464.6 | 8,661,281,021.05 |
| **Jumla Ndogo** | - | 10.0 | - | - | 25,095,485,556.50 | 126,819,795,464.6 | 151,915,281,021.05 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **KUSINI UNGUJA** | | | | | | | |
| Kati | 28,421,000.00 | 5.0 | 0.00 | 0.00 | 35,115,505,984.00 | 3,500,000,000.00 | 38,643,926,984.00 |
| Kusini | 32,197,975.00 | 6.0 | 0.00 | 0.00 | 22,452,548,621.00 | 4,829,602,536.00 | 27,314,349,132.00 |
| **Jumla Ndogo** | 60,618,975.0 | 11.0 | - | - | 57,568,054,605.0 | 8,329,602,536.0 | 65,958,276,116.0 |
| **MJINI MAGHARIBI** | | | | | | | |
| Mjini | 6,500,000.00 | 10.0 | 0.00 | 0.00 | 27,539,296,770.4 | 0.00 | 27,545,796,770 |
| Magharibi A | 10,000,000.00 | 7.0 | 0.00 | 41,920,900.0 | 10,923,188,537.6 | 43,022,917,484.0 | 53,998,026,922 |
| Magharibi B | 12,300,250.00 | 8.0 | 3,209,660,425.00 | 0.00 | 73,209,745,766.52 | 97,883,600.00 | 76,529,590,041.5 |
| **Jumla ndogo** | 28,800,250.00 | 25.0 | 3,209,660,425.00 | 41,920,900.0 | 111,672,231,074.5 | 43,120,801,084.0 | 158,073,413,733.5 |
| **JUMLA KUU** | **89,419,225.00** | **78.0** | **3,356,232,625.0** | **41,920,900.0** | **234,988,997,391.7** | **179,424,444,084.55** | **417,901,014,226.3** |

**Kiambatanisho no 3A**

**ORODHA YA VIJANA NA VIKUNDI VYA MAENDELEO YA VIJANA VILIVYOPATIWA MSAADA MBALI MBALI**

| S/N | Taasisi | Vikundi | Vijana | Aina ya msaada | Thamani ya Fedha | Vifaa | Thamani ya Vifaa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | PIRO | | 40 | vifaa | | incubator, mafriji, mipira, matank ya maji na sollar panel | 44,460,000 |
| 2 | SOS | | 10 | vifaa | | Vyerahani vya juki 7 na overloki 3 | 7,800,000 |
| 3 | USAID | | 5 | | 40,000,000 | | |
| 4 | Uchumi wa Buluu | 1 | 14 | Vifaa | | Boti ya kuvulia 1 na vifaa vyake | 25,000,000 |
| 5 | Uchumi wa Buluu | 1 | | vifaa | | Vifaranga vya kuku 162 | 370,000 |
| 6 | Feed the Future | 16 | 100 | Vifaa | | Mashine za ujasiriamli mbali mbali | 100,000,000 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | CYD | 1 | | | 10,000,000 | | |
| 7 | Mwakilishi na Mbunge jimbo Mtambile | 1 | | Vifaa | 300,000 | Tank lamaji 100L | 300,000 |
| 8 | Baraza la Vijana | 12 | | Vifaa | | Vifaa vya kilimo, ushoni na stationery | 12,000,000 |
| | **JUMLA** | **32** | **169** | | **50,300,000** | | **189,930,000** |

**KIAMBATANISHO NO 3B**

**Mchanganuo wa Usambazaji wa Sera ya Maendeleo ya Vijana Zanzibar 2023**

| S/N | Idadi ya wadau waliosambaziwa Sera | | | Aina ya wadau |
|---|---|---|---|---|
| | Ke | Me | Jumla | |
| 1 | 39 | 44 | 83 | Viongozi na watendaji wa Serikali |
| 2 | 394 | 321 | 715 | Asasi zisizo za Serikali |
| 3 | 1,413 | 755 | 2,168 | Vijana |
| **Jumla** | **1,846** | **1,120** | **2,966** | |

### *KIAMBATANISHO NAM: 2 MCHANGANUO WA VIKUNDI UNGUJA*

| S/N | Wilaya | Idadi ya vikundi vilivyote mbelewa | W'ke | W'me | Jumla | Idadi ya vikundi vilivyopata mikopo | Kiwango cha mkopo walichopata | W'ke | W'me | Jumla | Vikundi vilivyoomba mkopo | Thamani ya mkopo walioomba | Idadi ya Vikundi vipya | W'ke | W'me | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Wilaya ya mjini | 24 | 42 | 93 | 135 | 1 | shilingi milioni 18 (kikundi cha kwa pamoja tunaweza milioni 18 | 4 | 6 | 10 | 21 | 450,000,000 | 5 | 26 | 22 | 48 |
| 2 | Wilaya ya Magharibi 'A' | 27 | 106 | 66 | 172 | | | | | | 7 | 117,300,000 | 25 | 1308 | 993 | 2,301 |
| 3 | Wilaya ya Magharib | 39 | 45 | 55 | 100 | 4 | Shilingi Milion 24 kwa vikundi 4 | 10 | 14 | 24 | 17 | 440,000,000 | 40 | 2032 | 1986 | 4,018 |

| | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | i 'B' | | | | | | ambapo vikundi 3 kila kikundi milioni 3 (Kikundi cha ufugaji wa ngombe wa maziwa, upambaji na kilimo cha mboga mboga na Inua Vijana na Tehama milion 15) | | | | | | | | |
| 4 | Wilaya ya Kati | 15 | 23 | 56 | 79 | | | | | | | | | | |
| 5 | Wilaya ya Kusini | 5 | 32 | 26 | 58 | 1 | Shilingi milioni 3 (kikundi cha kilimo Wajibika) | 5 | 4 | 9 | 2 | 27,000,000 | | | |

| | | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 6 | Wilaya ya Kaskazini 'A' | 27 | 57 | 64 | 121 | | | | | | | | | | | |
| 7 | Wilaya ya Kaskazini'B' | 10 | 62 | 58 | 120 | 2 | Shilingi milion 9 (utambuzi coop milion 3 na mdogo mdogo cooperativ milion 6) | 6 | 10 | 16 | 10 | 242,500,000 | 12 | 38 | 76 | 114 |
| | **Jumla** | **147** | **367** | **418** | **785** | **8** | **54,000,000.00** | **25** | **34** | **59** | **57** | **1,276,800,000** | **82** | **3404** | **3077** | **6481** |

*MCHANGANUO WA VIKUNDI PEMBA*

| S/N | Wilaya | Idadi ya vikundi vilivyotembelewa | W'ke | W'me | Jumla | Idadi ya Vikundi vilivyopata mkopo | Kiwango cha mkopo walichopata | W'ke | W'me | Jumla | Vikundi vilivyoomba mkopo | Thamani ya fedha iliyoombwa | Idadi ya vikundi vipya | W'ke | W'me | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Chake Chake | 37 | 109 | 173 | 282 | 9 | Shilingi Milioni 92 Vikundi 9, (Kikundi cha Hope group shilingi milioni 5, Tujikomboe shilingi milioni 5, Kikundi cha Tawakal shilingi milioni 12, Wauzaji yebo yebo shilingi milioni 15, Tunaweza shilingi milioni 15, Kikundi cha Malaika shilingi milioni 15, Nia moja Wara shilingi milioni 5, Mtarazak shilingi milioni 10, Kitunze kidumu shilingi milioni 10. | 19 | 49 | 68 | 36 | 305,932,000 | 20 | 53 | 103 | 156 |

| | | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2 | Mkoani | 35 | 190 | 125 | 315 | 5 | Shilingi Milioni 75 vikundi 5 (kikundi cha Nia njema milioni 15, Mwanamke kazi co-operative milioni 15, Abifarm co-operative milioni 15,Tuzingatieni milioni 10 na Umoja ni nguvu milioni 20. | 8 | 27 | 35 | 10 | 184,000,000 | 18 | 190 | 125 | 315 |
| 3 | Wete | 38 | 210 | 246 | 456 | 4 | Shilingi milioni 72 na laki 5 vikundi 4, (Kikundi cha Ahsam production milioni 22, K- oficial group milioni 15, Pemba Farm milioni 20 na laki 5, Wete vegetable milioni 15. | 58 | 69 | 127 | 13 | 269,500,000 | 100 | 600 | 900 | 1500 |
| 4 | Michewe ni | 40 | 468 | 252 | 720 | 1 | Kikundi cha songa mbele shilingi millioni 10 | 3 | 5 | 8 | 3 | 55,000,000 | 8 | 38 | 42 | 80 |
| | **Jumla** | **150** | **977** | **796** | **1773** | **19** | **249,000,000** | **88** | **150** | **238** | **62** | **814,432,000** | **146** | **881** | **1,170** | **2,051** |